SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI NA MATUKIO GAZETI

Kila Mwezi

Septemba 28, 2019

Gazeti la Reli | Toleo Namba 2 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli akipata Maelezo kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alipotembelea Banda la TRC katika maonesho ya SADC katika kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha J.K Nyerere.

## RAIS MAGUFULI NA RAIS MUSEVENI WATEMBELEA BANDA LA TRC KATIKA KONGAMANO LA BIASHARA KATI YA TANZANIA NA UGANDA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda watembelea banda la Reli Tanzania - TRC na kujionea huduma na Miradi inayosimamiwa na TRC katika siku ya ufunguzi wa kongamano la kwanza la biashara kati ya Tanzania na Uganda katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha J.K Nyerere jijini Dar es Salam Septemba, 2019.

*Shirika la Reli Tanzania – TRC kubeba maono ya maendeleo ya uchumi wa nchi za SADC*



>> Uk. 2



*Dkt. Hassan Abbasi aipongeza TRC kwa kutangaza vyema miradi na huduma zitolewazo*

>> Uk. 3



*TRC na DIT zaingia makubaliano kuboresha matumizi ya teknolojia katika huduma za usafiri*

>> Uk. 4

*Uchorongaji milima kwa ajili ya ujenzi wa mahandaki ya reli ya kisasa waendelea; Zaidi ya Mita 470 zachorongwa*



>> Uk. 5

*Mabalozi kutoka nchi 42 Duniani wafurahishwa na kasi ya mradi wa SGR*



>> Uk. 6

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA – TRC KUBEBA MAONO YA MAENDELEO YA UCHUMI WA NCHI ZA SADC

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1

Banda la Shirika la Reli Tanzania -TRC limepata bahati kutembelea na mgeni rasmi Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Kassim wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Tehama, Habari, Uchukuzi na Hali ya Hewa wa nchi 16 za Jumuiya ya maendeleo ya kusini mwa Afrika – SADC, Mkutano huo umefanyika katika kituo cha mikutano cha kimataifa cha Julius Nyerere – JNICC hivi karibuni Septemba 2019 jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo ulianza Septemba 16, 2019 ambapo Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe alifungua rasmi mkutano kwa kuanza na makatibu wakuu wa Wizara zilizoshiriki mkutano huo uliokuwa na lengo la kuhakikisha kuwa na soko la pamoja katika sekta ya miundombinu ya uchukuzi na mawasiliano ifikapo mwaka elfu mbili na hamsini (2050) sekta hizo ambazo ni mhimili mkubwa katika kufikia azma ya maendeleo katika jumuia hiyo iliyodumu kwa zaidi ya miongo miwili na nusu.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Kassim alifika katika banda la Shirika la reli Tanzania - TRC na kupokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa na kupewa maelezo kuhusu maendeleo ya miradi mikubwa ya kitaifa inayosimamiwa na Shirika la Reli ikiwemo ujezi wa reli ya kisasa - SGR na uboreshaji wa reli ya kati – TIRP, pamoja na miradi mingine kama ufufuaji wa njia ya reli Dar es - Salaam - Moshi - Arusha.

Mkurugenzi Mkuu alisisitiza endapo miundombinu ya reli ikiimarishwa itasaidia kukuza uhusiano kwa kutoa fursa za kibiashara ndani ya jumuiya ya nchi za SADC.

Aidha, katika mkutano huo Waziri Mkuu amebainisha mchango wa ujenzi wa reli ya kisasa sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya reli katika kuleta maendeleo ya uchumi kwa wanachama wa jumuiya ya SADC. "kati ya miradi mikubwa inayotekelezwa hapa Tanzania ni ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendokasi inayojengwa katika ukanda wa kati pamoja na ukanda wa reli ya TAZARA ambayo inaunganisha nchi za wanachama wa SADC, reli hizi zitaboresha biashara kati ya Tanzania na nchi za wanachama wa SADC" alisema Waziri Mkuu.

Kwa upande wake Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe ambaye ni Mwenyekiti wa kamati ya mawaziri wa wizara hizo, amezungumzia juu ya mpango wa jumuiya hiyo katika kuleta maendeleo katika nchi hizo ikiwemo sekta ya uchukuzi kwa njia ya reli "wajumbe wameleta hoja mbalimbali zikiwemo namna za kushughulikia ujenzi wa miundombinu kama vile Reli, kukabiliana na majanga pamoja na hali ya hewa, manufaa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha uchumi wa SADC, wataalam kutoka sekta za kibenki wameeleza uwezo wao katika kusaidia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu katika SADC" alisema Waziri Kamwelwe.




*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kushoto) akimuelezea Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim kuhusu Maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR alipotembelea banda la TRC katika kituo cha JNICC jijini Dar es Salaam Septemba 2019*

## MSEMAJI MKUU WA SERIKALI DKT. HASSAN ABBASI AIPONGEZA TRC KWA KUTANGAZA VYEMA MIRADI NA HUDUMA ZA TRC

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1

Msemaji Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo Dkt. Hassan Abbasi ametembelea Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa lengo la kutoa elimu kuhusu muongozo na Mkakati wa Mawasiliano ya Shirika pamoja na kujionea maendeleo ya ujenzi wa stesheni ya reli ya kisasa – SGR jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Msemaji Mkuu wa Serikali alipata fursa ya kuelezea miongozo ya mawasiliano ndani na nje ya shirika kwa kuwa upo umuhimu wa kuweka miongozo juu ya nani wa kuzungumza, nini cha kuzungumza na kwa wakati gani.Pia ili kuhakikisha mawasiliano na habari vinakwenda sambamba Msemaji Mkuu amesisitiza suala la ushirikiano kati ya Idara na Vitengo ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa umma na kwa wakati. Dkt. Abbasi amekipongeza kitengo cha Habari na Uhusiano TRC kwa kazi kubwa ya kutoa habari kwa umma kuhusu maendeleo ya miradi pamoja na huduma zinazotolewa na shirika, pia amesisitiza kitengo cha habari na uhusiano kuendelea kuitangaza miradi ya shirika ili wananchi waweze kuona na kuelewa maendeleo yanayofanywa na serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedari Dk. John Pombe Magufuli.

"tunaona kazi kubwa ya kitengo cha Habari na Uhusiano, sio leo ipo siku mtakumbukwa, nafurahi viongozi wanaona na sisi tunaosimamia tunapata mrejesho, hongereni sana" aliongeza Dkt. Abbasi

Aidha, Dkt. Abbasi amebainisha umuhimu wa kutoa habari kwa umma kwa wakati sahihi kwa kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi za wananchi katika Miradi na namna pekee ya kuujulisha umma matumizi ya pesa hizo ni kupitia habari na mawasiliano ya kimkakati kwa umma. "kuisemea serikali na kuitangaza miradi ya serikali ni kitu kikubwa sana na muhimu kwa serikali na taasisi" alisema Dkt. Abbasi

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amemshukuru Dkt. Abbasi kwa ujio wake na kutoa elimu ya muongozo wa mkakati wa mawasiliano utakaoliwezesha shirika kutoa taarifa kwa utaratibu mzuri bila kuwepo athari kwa shirika na umma kwa kuepuka upotoshaji wa taarifa muhimu, Mkurugenzi pia amewataka wakuu wa Idara na Vitengo kufuata muongozo huo katika mawasiliano ya kila siku kwa kushirikiana na kitengo cha Habari Uhusiano ili kuleta ufanisi katika mawasiliano

"Suala la 'mawasiliano sio suala tu la kuzungumza, bali lina maana kubwa kwenye taasisi na katika taifa" alisema Kadogosa



*Meneja Msaidizi Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Ayoub Mdachi akimfafanulia Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi (wa pili kushoto) kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Stesheni ya Reli ya Kisasa ambayo ujenzi wake umefika zaidi ya asilimia 80 eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam hivi karibuni.*

Aidha Dkt. Abbas alipata fursa ya kitembelea eneo la Stesheni na kujionea maendeleo ya Ujenzi wa Stesheni kubwa ya reli ya kisasa jijini Dar es Salaam pamoja na daraja lenye urefu wa KM 2.5 litakalotumika kupitisha treni za umeme kuanzia Stesheni ya Dar es Salam hadi Ilala ili kuepusha msongamano wa magari na watembea kwa miguu.



*Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi (mwenye tai) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania alipotembelea ofisi ya Makao makuu TRC jijini Dar es Salaam hivi karibuni.*

## TRC NA DIT WAKUBALIANA KUSHIRIKIANA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1




*Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kulia) na Mkuu wa tasisi ya DIT Prof. Preksedis Ndomba (kushoto) wakitiliana saini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano wa mafunzo, utafiti na matumizi ya teknolojia katika huduma za usafiri wa reli, katika ofisi ya makao makuu ya TRC Dar es Salaam*

Shirika la Reli Tanzania – TRC limetiliana saini mkataba na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – DIT kwa lengo la kushirikiana katika kutoa mafunzo, kufanya utafiti, na kuendeleza matumizi ya teknolojia katika sekta ya reli.

Makubaliano hayo yametiliwa saini kati ya Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa na Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Prof. Preksedis Ndomba pamoja na wanasheria kutoka pande zote mbili ambapo hafla hiyo imehudhuriwa na Wakuu wa Idara kutoka TRC, wawakilishi kutoka DIT na wanahabari katika ukumbi wa Ofisi ya Makao Makuu TRC Dar es Salaam Septemba 11, 2019.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania ameeleza dhumuni la makubaliano hayo kuwa ni kutokana na mabadiliko yanayotarajiwa kutokea katika Shirika hususani katika huduma. Amesema matumizi ya teknolojia ni muhimu kwa kuwa Shirika linasimamia miradi mikubwa ukiwemo wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR, Uboreshaji wa Reli ya Kati – TIRP na ukarabati wa Mabehewa hivyo kuwa na wataalamu watakaoleta chachu ya matumizi ya teknolojia ni muhimu.

"TRC tuko kwenye mageuzi na mageuzi yanakuja na teknolojia na vitu vipya, tunajenga reli ya kisasa – SGR kwahiyo tunahitaji kujua mifumo ya uendeshaji jinsi ilivyo kwahiyo sisi tumelikaribisha hili" alisema Kadogosa

Prof. Ndomba amesema kuwa hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo alizitaka taasisi, Mashirika na serikali kufanya mageuzi ya teknolojia hivyo DIT ikaamua kuzishirikisha taasisi, serikali na makampuni katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi wake, pia amesema kuwa TRC ni taasisi ya kimkatati kwa ajili ya kujifunza

## TIMU YA MAWASILIANO TRC KUFANYA KAMPENI YA UELEWA KUHUSU MIRADI, HUDUMA NA USALAMA WA RELI DAR - ISAKA

Shirika la Reli Tanzania - TRC linatarajia kufanya Kampeni ya Uelewa kuhusu Huduma na Miradi inayosimamiwa hususani Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR na Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka hivi karibuni 2019.

Timu ya Mawasiliano itakayohusika katika kampeni hiyo itajumuisha wataalam kutoka Idara mbalimbali za TRC zinazohusika moja kwa moja na Miradi na Huduma zitolewazo lengo kuu likiwa ni kutoa elimu juu ya namna ya kujikinga na athari za Miradi, ulinzi wa Miradi na Miundombinu ya Reli, namna ya kutumia fursa zitokanazo na Miradi na Huduma za Shirika, pia timu hiyo itakusanya Malalamiko, mapendekezo na Maoni kuhusu Miradi na Huduma zitolewazo na TRC.

Aidha Shirika litakutana na kuwasiliana na Wananchi hususani wanaoishi maeneo ambayo reli na Miradi ya reli inafanyika kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka kupitia Mikutano ya Wananchi katika Vijiji na Vitongoji pia kupitia vyombo vya habari vilivyopo katika maeneo husika.

Timu ya Mawasiliano kutoka TRC itashirikiana na Vyombo vya Usalama, Viongozi wa maeneo husika ambao ni Wakuu wa Wilaya, Mikoa, Tarafa, Kata, Vitongoji na Vijiji husika.

# UCHORONGAJI MILIMA KWA AJILI YA UJENZI WA MAHANDAKI YA RELI YA KISASA WAENDELEA

Na Mwandishi wetu TRC

>> Inatoka Uk. 1




Mlango wa kutokea wa Handaki la 2 kati ya Mahandaki 4 yanayojengwa kupitisha reli ya Kisasa - SGR eneo la Kilosa mkoani Morogoro

Shirika la Reli Tanzania - TRC laendelea na usimamizi wa Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Kilosa mkoani Morogoro, ambapo kazi kubwa katika eneo hilo ni uchorongaji Milima kwa ajili ya ujenzi wa mahandaki 'tunnels' yatakayopitisha reli ya Kisasa kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo la Milima ya Kilosa na Mto Mkondoa mkoani Morogoro, Septemba 2019.

Mahandaki 4 yenye jumla ya urefu wa KM 2.6 yanatarajiwa kujengwa katika Mradi wa SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo la Kilosa huku handaki refu zaidi nchini likiwa na urefu wa KM 1.031 ili kuepuka athari za mto Mkondoa ambao umekuwa ukifurika kipindi cha mvua kubwa na kuathiri miundombinu ya reli ya 'Meter Gauge'.

Hata hivyo ujenzi wa awamu ya pili ya reli ya SGR kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutupora Mkoani Singida, ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 15, huku kazi ya kuandaa tuta na madaraja ikiendelea lakini kubwa zaidi ni kazi ya uchorongaji wa mahandaki yapatayo manne, likiwemo hili lenye urefu wa kilomita moja.

Mhandisi Amiri Khamis Mkaguzi wa mahandaki kutoka Kampuni ya KORAIL ambao ni washauri wa ujenzi wa mradi amebainisha kuwa kazi ya uchorongaji Milima inaendelea kwa kasi ambapo zaidi ya Mita 16 huchorongwa kwa siku. Mpaka sasa zaidi ya mita 470 kati ya Mita 1031 zimechorongwa huku kazi ya uchorongaji ikiwa imefikia zaidi ya asilimia 45. Aidha, kazi ya ujenzi wa mahandaki inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2019.

Bi. Catherine Kipeja Mtaalamu wa kuangalia ubora wa kazi katika ujenzi wa handaki amezungumzia namna kazi ya ujenzi inavyozingatia ubora wa zege linalotumika katika ujenzi wa handaki hilo.

"kazi yetu ni kupima ubora wa zege, tunapima joto la zege ambalo linatakiwa lisizidi nyuzi joto 32, mmiminiko wa zege usiwe chini milimita 100 ndipo mhandisi huruhusu gali la zege lipelekwe ndani" alisema Bi. Catherine.

**"Mpaka sasa zaidi ya mita 470 kati ya Mita 1031 za handaki namba 2 zimechorongwa huku kazi ya uchorongaji ikiwa imefikia zaidi ya asilimia 45"**

# MABALOZI WA TANZANIA KUTOKA NCHI 42 DUNIANI WAFURAHISHWA NA KASI YA MRADI WA RELI YA KISASA

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1

Shirika la reli Tanzania - TRC lapokea Ugeni wa mabalozi wa Tanzania takribani 42 kutoka nchi mbalimbali Duniani wakiwemo Mabalozi kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika - SADC ambao wametembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Dar es Salaam – Morogoro hivi karibuni.

Ugeni huo ulipokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa katika eneo ambalo stesheni kubwa ya reli ya kisasa inajengwa jijini Dar es Salaam na kuwapa maelezo kuhusu ujenzi wa SGR ambao ulianza 2017 chini ya Mkandarasi Yapi Merkezi ambapo mradi unatekelezwa kwa kusanifu na kujenga.

Ndugu Kadogosa alielezea faida za Mradi zikiwemo ajira ambapo 96% ya wafanyakazi ni Watanzania, Mkurugenzi ameeleza kuwa shirika linaendelea na mpango wa kuandaa vijana watakaosimamia na kuendesha shughuli za usafirishaji katika reli ya kisasa ambapo vijana hao wanapewa mafunzo ya nadharia na vitendo nje na ndani ya nchi ili mradi utakapokamilika kuwe na nguvukazi ya kuweza kuendeleza mradi huo mkubwa.

"Katika miradi mikubwa inayosimamiwa na Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Mh. Rais Dr.John Pombe Magufuli Ujenzi wa Reli ya Kisasa ni mmoja wapo" alisema Ndugu Kadogosa.

Vivyo hivyo Mkurugenzi Mkuu wa TRC alitolea ufafanuzi kuhusu tofauti



*Balozi wa Tanzania nchini Uganda Mhe. Dkt. Aziz Mlima (kushoto) na Balozi wa Tanzania nchini Sweden Mhe. Dkt. Wilbroad Slaa (kulia) wakifurahia safari na treni ya uhandisi wakati wa ziara ya Mabalozi kuona Mradi wa SGR hivi karibuni 2019.*

zilizopo kati ya Reli ya kisasa - SGR inayojengwa Tanzania na za nchi nyingine barani Afrika na kusema kuwa reli inayojengwa nchini ni ya kipekee kuwahi kujengwa Afrika

aliongeza kuwa reli ya kisasa ya Tanzania itakuwa na uwezo mkubwa wa ekseli 35 tofauti na nchi zingine ambazo nyingi ni 25. Mizigo itakayobebwa ni pamoja na madini kutoka Kongo na Msongati Burundi.

Mwendokasi kwa treni ya mizigo utakuwa 120 na 160 kwa treni za abiria ambayo kitaalamu ni 'single truck' hivyo ni tofauti na reli nyingine.

Mabalozi walipata Fursa ya kupanda treni ya majaribio ya mkandarasi kuanzia stesheni ya Soga hadi Kikongo mkoani Pwani ambapo mabalozi walifurahishwa na ubora na uimara wa reli kwa kuwa haina mitikisiko kama ilivyozoeleka katika reli ya 'Meter Gauge', pia Mkurugenzi aliwashukuru Mabalozi hao kwa kuwa anaamini watakuwa mabalozi wazuri "Najua mtakuwa mabalozi wazuri kwa nchi mnazofanyia kazi" alisema Mkurugenzi Mkuu wa TRC.

Akizungumza na waandishi wa Habari Balozi wa Uingereza Dkt. Asha Rose Migiro ameipongeza serikali ya Tanzania kwa utekelezaji wa Mradi wa SGR kwa kuwa Mabalozi ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa nchi hivyo uwepo wa Miundombinu imara ya reli, anga, barabara na bandari unaleta matumaini makubwa katika kuleta uchumi imara

"Tunapotekeleza diplomasia ya uchumi, miundombinu ni lazima hivyo uwepo wangu kwenye treni hii ni ndoto iliyotimia, nampongeza Rais wa Jamhuri na Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kungu Kadogosa kwa usimamizi mzuri" alisema Dkt. Asharose Migiro

Mabalozi pia walitembelea kiwanda cha mataruma kilichopo Soga mkoani Pwani ambapo kiwanda hicho kinazalisha mataruma 1500 kwa siku, mabalozi pia walisifu ubora wa mataruma hayo.

# UTEKELEZAJI

## UBORESHAJI WA RELI YA KATI DAR - ISAKA WAENDELEA




*Kazi ya kuweka reli juu ya tuta lililofanyiwa maboresho ya udongo (Soil Improvement) ikiendelea eneo la Kintinku mkoani Singida hivi karibuni Septemba 2019*



*Mafundi wakipima upana wa reli ili kuhakikisha usawa wa vipimo kutoka reli moja na nyingine mara baada ya mtambo maalum wa kushindilia kokoto kupita juu ya reli eneo la Makutupora Singida hivi karibuni Septemba 2019..*



*Muonekano wa moja ya Madaraja makubwa yaliyofanyiwa maboresho hivi karibuni Septemba 2019*



*Muonekano wa sehemu ya kipande cha reli ambacho kimefanyiwa ukarabati eneo la Mombasa jijini Dar es Salaam hivi karibuni Septemba 2019*

# *Picha zikionesha Maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Morogoro - Makutupora ambao umefikia zaidi ya 15%*




*Mtambo ukichoronga Mlima ili kupata Handaki la pili lenye urefu wa Mita 1030 Kilosa mkoani Morogoro*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya kufunga nondo katika kuta za handaki*



*Mtaalamu akiendelea na kazi ya kuweka zege. Zege hupimwa ili kuhakikisha linakidhi viwango kabla ya kuwekwa katika kuta za handaki.*



Muonekano wa sehemu iliyochorongwa Mita tatu (3) kwenda chini na kuwekwa zege ili kuimarisha handaki.



Maandalizi kwa ajili ya hafla ya uzinduzi wa kazi ya utandikaji wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Morogoro - Makutupora Singida yanaendelea katika eneo la Parakuyo wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro. Katika picha tuta linaonekana likiwa tayari kwa ajili yakuweka mataruma na kutandika reli vyote vikiwa pembezon mwa tuta



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kushoto) na Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - DIT Prof. Preksedis Ndomba wakionesha Mkataba wa Makubaliano ya ushirikiano wa Mafunzo na Uendelezaji wa Matumizi ya teknolojia katika huduma za usafiri wa reli mara baada ya kutiliana saini makubaliano hayo katika ukumbi wa ofisi ya makao makuu TRC Dar es Salaam Septemba 2019.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia Afrika Kanda ya Afrika Bi. Anne Kabagambe (wa pili kushoto) akitazama reli ya Kisasa - SGR iliyotandikwa eneo la Vingunguti jijini Dar es Salaam Agosti 2019




Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mhandisi Machibya Masanja akimuelezea Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu nchini Rwanda Mhandisi Patricia Uwase (wa pili kulia) kuhusu Maendeleo ya Ujenzi wa Stesheni ya SGR eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam Septemba 2019.



Meneja Msaidizi Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mhandisi Ayoub Mdachi akifafanua kuhusu Maendeleo ya Ujenzi wa Stesheni ya SGR kwa Madiwani na viongozi kutoka Manispaa ya Singida waliotembelea mradi wa SGR eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam Septemba 2019.

# UKARABATI WA MABEHEWA – TRC KUWA CHACHU YA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI KUPITIA USAFIRISHAJI WA MIZIGO

Na Mwandishi wetu TRC



Katika miaka ya hivi karibuni tangu Rais wa awamu ya tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aingie madarakani, ajenda kuu ya serikali ya Tanzania ni kuifanya Tanzania kuelekea uchumi wa kati na kuwa Tanzania ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Agenda hiyo imelenga kusisitiza mipango ya ukuaji na uboreshaji wa miundombinu wezeshi ikiwemo reli ili kuongeza ufanisi katika utendaji sambamba na kuhakikisha Tanzania inatimiza lengo la ukuaji wa uchumi na viwanda. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uwekezaji wa miundombinu wezeshi ya kiuchumi katika usafirishaji ambayo ni barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 252.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli kupitia Mfuko wa Reli haya yote yanafanyika Ili kuimarisha miundombinu katika sekta ya usafirishaji wa reli nchini kwa maslahi ya Taifa.

Maono ya Shirika la Reli Tanzania – TRC ni kutoa huduma bora, salama na ya kuaminika katika usafiri wa Reli Afrika Mashariki na Kati. Sanjari na maono hayo Shirika limejikita hasa kusimamia usafirishaji wa reli kwa gharama nafuu, utunzaji wa miundombinu ya reli na utoaji wa huduma za usafiri wa uhakika na salama kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Tanzania.

Ili kutimiza dhamira ya utendaji kazi kwa ufanisi shirika linaendelea kuboresha miundombinu ya reli kwa ili kuendeleza na kuhakikisha usafiri wa reli nchini unakuwa wa uhakika zaidi na kuchochea uchumi wa nchi kupitia sekta ya usafirishaji na uchukuzi katika kipindi hiki cha mchakato wa ujenzi wa viwanda nchini.

Jitihada zimeendelea kufanyika ambapo Serikali imekuwa ikiliwezesha Shirika kwa kutoa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya reli ili kuongeza ufanisi katika utendaji na sasa imeelekeza nguvu katika ukarabati wa mabehewa ambayo kwa muda mrefu yalikuwa yamechakaa na mengine kuharibika kutokana kukaa kwa muda mrefu bila kutumika.

Mapema, mwaka 2019 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli Kupitia Wizara ya Uchukuzi alitoa kiasi cha Shilingi bilioni 4 kwa TRC kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 200 ya mizigo kwa dhumuni la kuongeza ufanisi katika huduma ya usafirishaji mizigo nje na ndani ya nchi kwa lengo la kupunguza mrundikano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza makusanyo ya Shirika. Mradi huu wa ukarabati wa mabehewa utasaidia kwa kiasi kubwa kuboresha ufanisi na kuleta faida kwa watanzania.

kwa kawaida behewa hufanya kazi zaidi ya miaka 6 bila kufanyiwa matengenezo makubwa endapo halitapata ajali. Ukarabati wa behewa TRC uhusisha mfumo mzima wa behewa ukiwemo uboreshaji wa muonekano wa behewa (bodi) mfumo wa breki, baada ya kumaliza uboreshaji wa mfumo mzima behewa hupakwa rangi. Kwa hivi sasa kazi ya ukarabati wa mabehewa inafanyika katika karakana kuu ya Reli jijini Dar es Salaam ambapo mafundi wa kila kitengo hufanya kazi zao kwa wakati, hivyo kupelekea kukarabati mabehewa matano (5) kwa wiki moja na kwa mwezi hukarabati mabehewa ishirini (20).

Gazeti la Reli na Matukio limezungumza na Mkurugenzi anayesimamia Mabehewa na Vichwa vya treni Mhandisi Albert Magandi ambaye amesema kuwa kazi kubwa inayoendelea ni ukarabati wa mabehewa yanayokidhi mahitaji ya wateja kulingana na aina ya shehena ya mzigo unaotakiwa kusafirishwa.

Mabehewa yanayofanyiwa ukarabati ni CCB (Container Carrier Bogie) - hubeba makontena, HLB(C) (High Large Bogie) - hubeba makontena, mabomba, mbao, magogo, na vyuma, CLB (Covered Large Bogie) - hubeba mizigo ya jumla kama vile Saruji, Sukari, Chumvi, Kahawa, Pamba, Tumbaku. BHB (Ballast Hopper Bogie) - hubeba kokoto, PTB (Petroleum Tank Bogie) - hubeba mafuta MGB (Motor Goods Bogie) - hubeba magari, CWB (Cattle Wagon Bogie) - hubeba mifugo. Aina hizi za mabehewa zitakapokamilika zitasaidia kusafirisha mizigo ndani ya Tanzania na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kupitia bandari ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Tanga.

“mpaka sasa mebehewa 80 yamekarabatiwa na yanafanya kazi na mengine yako katika hatua mbalimbali za ukarabati, mradi wa ukarabati wa mabehewa 200 unatarajiwa kukamilika Disemba 2019” alisema Mhandisi Magandi.

Serikali ina jukumu la kusimamia maendeleo ya uchumi, kwa maana hiyo, moja ya madhumuni ya kiuchumi ni kutekeleza sera madhubuti ili kuhakikisha kuwa miundombinu sahihi ya usafirishaji inasaidia upatikanaji wa bidhaa na malighafi kwa bei nafuu na kukuza uchumi wa nchi. Kukamilika kwa Mradi huu awamu ya kwanza kutasaidia katika kukuza sekta za Maendeleo ikiwemo kilimo, viwanda, biashara, uwekezaji na mawasiliano nchini.

Serikali ina mpango endelevu wa kukarabati mabehewa 700 hadi 1000 ili shirika liweze kubeba mizigo inayoingia bandari ya Dar es Salaam na kusafirisha sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ufanisi.

Hata hivyo kuna hitaji kubwa la Mabehewa ya kutosha kutokana na idadi na mizigo iliyopo Bandari ya Dar es Salaama na sehemu nyingine, pia uwepo wa miradi ya uboreshwaji wa miundombinu ya reli ni kiashiria tosha cha hitaji la Mabehewa na vichwa vya kutosha vitakavyofanya kazi katika reli inayoboreshwa kupitia mradi wa uboreshaji wa reli ya kati Tanzania - TIRP.

Uwekazaji unaondelea katika sekta ya Reli nchini inaonesha dhahiri Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedali, Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kuwa chachu katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kutekeleza dhamira ya Tanzania kua ya Viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

## AFYA INAVYOPEWA KIPAUMBELE KATIKA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR

Na Dkt. Apolinary John



Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuzidi kutubariki sisi Watanzania ambao kwa Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais mpendwa Mhe. Dkt. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI. Mimi kama mtaalamu wa Afya maeneo ya kazi (Occupational Physician) ninapenda kutumia uwanja huu kuwahabarisha wafanyakazi wenzangu wa kada zote kwamba miradi kama hii mikubwa inayotekelezwa kwa kipindi hiki ni zawadi za kipekee kutoka kwa Mungu, na ni kitu cha kujivunia.

Azma ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mchapakazi Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli ni kuhakikisha Tanzania inafikia lengo la kuwa nchi yenye uchumi wa kati, kwa kuhakikisha hilo Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha na kujenga miundombinu mipya ikiwemo reli hii ya kisasa – SGR inayojengwa Dar es Salaam hadi Mwanza na maeneo mengine ya nchi. Kama ilivyo Miradi mingine nguvukazi ndio mtaji wa kwanza lakini nguvukazi haiwezi kuwa na tija endapo itakuwa dhoofu hivyo serikali inachukua hatua za awali kabisa katika kuhakikisha afya ya nguvukazi ili kutimiza malengo ya kitaifa katika Miradi mikubwa.

Kazi kubwa ya watoa huduma za afya kwa wafanyakazi ni kufanya uchunguzi wa kiafya tukishirikiana na hospitali za serikali na kujiridhisha kama watu wanaoomba kazi wana afya bora kulingana na majukumu watakayopewa katika kitengo husika. Zoezi hili ni endelevu; yaani kuna uchunguzi kabla ya kazi, ukiwa unaendelea na kazi na hata pale mradi utakapokwisha tutapenda kuona wafanyakazi wazalendo wa kitanzania wakiendelea kuwa na afya bora. Kwa kufanya hivi wafanyakazi walio na afya bora hupatiwa kazi na kama afya ilivyo mtaji wa kwanza katika ujenzi wa Taifa lolote, Watanzania tupo tunapiga kazi.

Miradi ndio kwanza inaanza, Tanzania bado ina safari ndefu mpaka kufikia ulimwengu wa kwanza. Moja kwa moja tujikite kukumbushana mambo ya msingi ambayo tulifundishwa na wakufunzi juu ya kujikinga na ajali zinazoweza kutokea katika maeneo ya kazi. Ni lazima kuangalia matumizi sahihi ya mavazi maalumu kazini 'Personal Protective Equipment' (PPE) na kuchukua tahadhari.

Kila kazi ina maelekezo yake ya namna bora ya kuifanya na mavazi yake maalumu. Kwa hiyo ni vema kuzingatia maelekezo yanayotolewa na watu wa usalama (HSE – Team) wanaokuwepo mara kwa mara katika maeneo ya kazi. Namna bora ya kupanda kwenye majukwaa ya ujenzi wa miundombinu iliyoinuka. Kuzingatia namna bora ya kunyanyua vitu vizito. Kutumia Maski kuziba mdomo na pua ili kuepuka kemikali na vumbi.

Uvaaji nguo maalumu (overall and reflector). Tunalazimika kuvaa nguo maalumu zinazoweza kuwa ngumu na nzito ili kuwa salama, naomba tusichoke kuzitumia. UZEMBE wako usiuendekeze kwa kujiita MZOEFU WA HIZI KAZI maana ajali zipo lakini zinaepukika kama tukiwa makini na kufuata maelekezo.

Miwani, viatu vyenye ngozi ngumu na chuma (safety boots), glavu (gloves) kwa ajili ya kuilinda mikono yetu, mikanda ya usalama (safety harness) na vingine vingi vinatolewa bure na kampuni ili kuwalinda wafanyakazi kulingana na mazingira na vitengo vyao vya kazi.

Nguo zenye kuakisi mwanga wa magari au mitambo nazo ni vema kuvaliwa wakati wote kazini. Tusione adhabu kuvaa na kutumia vifaa vya kutufanya kuwa salama wakati wote. Afya ni moja na haina ziada hivyo hatuna budi kuitunza kwa namna yoyote. Hata mtu mmoja akiumia au kupoteza maisha yake bado ni hasara kubwa kulingana na jinsi alivyotarajiwa kutimiza malengo yake katika ngazi ya familia, jamii, taifa lake na hata dunia.

Masuala ya afya na usalama wa mazingira ya kazi (HSE) yanapewa kipaumbele, elimu endelevu inatolewa mara kwa mara kulingana na uhitaji. Usalama huleta amani na amani huleta ufanisi wa kazi. Magari ya kubebea wagonjwa (ambulances) yapo kulingana na mahitaji na huduma ya bima ya afya (NHIF) ni kwa kila mfanyakazi. Afya ni kuwa vizuri kimwili, kiakili na kijamii. Tangu mwanzo tulitambua hayo na kuweza kuweka misingi mizuri mpaka sasa nasema tuko vizuri.



Ndugu Masanja Kungu Kadogosa
Mkurugenzi Mkuu TRC

## Neno kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

Ninapenda kutanguliza Shukurani za dhati kwa Mwenyezi Mungu ambaye ametupa nguvu sisi watendaji na amempa nguvu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutekeleza Miradi mikubwa ya kitaifa lakini pia kuiweka nchi yetu katika njia inayotupeleka katika Tanzania ya Viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025.


Kwa kipekee kabisa ninapenda kuwapongeza wafanyakazi wenzangu wa Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa utendaji na usimamizi mzuri wa Miradi hususani Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa, Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati pamoja na Mradi wa Ukarabati wa Mabehewa.

Miradi hii kwa pamoja inatupa nguvu na matumaini sisi kama watanzania katika safari yetu ya kuelekea Tanzania ya Viwanda na uchumi wa kati.

Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa TRC naahidi kwa Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania wote kuwa hatutawaangusha katika safari hii.

Zaidi nawasisitiza watanzania tuendelee kumuunga Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika kuthamini cha kwetu na kulinda miundombinu ya reli maana reli hii ni mali ya watanzania.

## MPANGO WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR DAR ES SALAAM - MWANZA





SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 70364
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042


Reli Yetu, Maendeleo Yetu, Taifa Letu #TRCMpya
tzrailways TRC Reli TV


Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Mohammed Mapondela |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |